# WILAYA YA NANDI
# DARASA LA TANO MUHULA WA TATU
PENPLUS NANDI
# KISWAHILI

Muda: Saa 1 Dakika 40

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze nafasi 1-15.**

Mvua ilipoanza ___1___ ___2___ walikuwa barabarani mjini. Ikabidi baba na mjukuu ___3___ kutafuta mahali karibu na maduka ___4___ na mvua. Waliona watu wengine wakitimua ___5___ muda tu mvua ilipoteremsha ___6___ zake kwenye uso wa ___7___. Kilichowashangaza ni kuwa watu hao waliogopa ___8___ lakini hawakuogopa kugongwa na ___9___.

"Babu, kwa nini wale wanawake wamejifunika karatasi ___10___ nailoni?" Mjukuu ilimtoka. "Mbona hiki ni ___11___ !"

"Wewe unafikiri wataziacha nywele ___12___ ziingie maji bure ___13___ na wamemwaga mamia ya pesa ___14___ saluni?" Babu alimtegulia kitendawili ___15___.

1. A. kunyesha B. kumwagika C. kutonyesha D. kupusa
2. A. pote B. kote C. wote D. mote
3. A. wake B. chake C. yake D. pake
4. A. waimbe B. waceke C. walale D. wajikinge
5. A. mbiu B. mbio C. miguu D. meno
6. A. njema B. sema C. pema D. neema
7. A. arthi B. bingu C. ardhi D. binguni
8. A. kuokota B. kukoka C. kwenda D. kula
9. A. magari B. meli C. ndege D. mashua
10. A. za B. wa C. la D. cha
11. A. vioja B. kioja C. kionja D. vionja
12. A. kwo B. pao C. zao D. nao
13. A. bure B. bilashi C. bilabila D. ovyo
14. A. kuzitema B. kuzilisha C. kuzipanda D. kuzitengeneza
15. A. yake B. wake C. pake D. chake

**Kuanzia nambari 16 - 30 jibu swali kulingana na maagizo.**

16. $^{2}/_{5}$ ni sawa na ________
    A. humusi mbili B. nusu tano
    C. theluthi mbili D. tusui tatu

17. Kamilisha semi hii;
    Aliponea chupu ________ katika ajali hiyo.
    A. chapu B. chupu
    C. churu D. chache

18. Yeye anaringa kama ________
A. paka B. simba
C. tausi D. sungura

19. Maneno kama kalamu, chupa na dawa yapo katika ngeli ya ________
A. U - I B. KI - VI
C. I - ZI D. LI - YA

20. Katika kusafiri kwenye basi watu hulipa ________
A. nawiri B. karo
C. kiingilio D. nauli

21. Tumia alama sahihi ya uakifisho.
"Kumbe Maria amefika ________
A. ? B. !
C. " D. _.

22. Wingi wa "kifaranga wangu" ni ______
A. Vifaranga vyetu
B. Vifaranga wao
C. Viraranga vyangu
D. Vifaranga wetu

23. Ni ala ipi ambayo si ya muziki?
A. Bisibisi B. Kayamba
C. Gitaa D. Kinubi

24. Andika sentensi hii kwa udogo.
Mji wetu ni mdogo sana.
A. Kijiji chetu ni kidogo sana.
B. Jiji letu ni dogo sana.
C. Kijiji chetu ni kijidogo sana.
D. Miji yetu ni ndogo sana.

25. Kanusha sentensi ifuatayo.
"Abdi anakula chakula".
A. Abdi hakuli chakula.
B. Abdi hakuli vyakula.
C. Abdi hali vyakula.
D. Abdi hali chakula.

26. Kutokana na jina 'msomaji' tunapata kitenzi ______
A. somo B. soma
C. usomaji D. masomo

27. Tumia kivumishi '-enye' vizuri.
Shamba ______ rutuba lina mavuno.
A. chenye B. mwenye
C. lenye D. yenye

28. Tunasema baraza la wazee, jozi la viatu na kicha cha ______
A. ndizi B. kuni
C. funguo D. askari

29. Nini maana ya;
Eli ni sungura ________?
A. baridi mno
B. yu mlafi
C. ni mkali
D. mjanja

30. Mmea wa mgomba huzaa ________
A. ndizi
B. kahawa
C. zabibu
D. miwa

**Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Siku iliyofuatia ya klabu, rafiki yangu nami tulikuwa tunatayarisha shamba la mbegu. Tulifanya shamba hilo ndogo la mbegu kuinukia kwa kuinua mchanga, kama vile Bw. Odhis alivyokuwa ametuonyesha mwaka uliopita. Ayaga, Kageha na mimi tulitayarisha shamba moja na wengine wa kikundi hicho wakichota nyasi zilizokauka. Kisha tulinyunyizia maji shamba na kuvuna mbegu zetu.

Tulivuna mbegu za nyanya, kabeji na karoti katika shamba tofauti. Baadaye

tulifunika vijishamba hivyo kwa nyasi zilizokauka na kumwaga maji mengi juu ya nyasi hizo. Mbegu hizo hazikuwa lazima zinyunyiziwe maji kwa siku kadhaa.

31. Ilikuwa ni siku gani kwa wanafunzi?
A. Siku ya klabu
B. Siku ya kuigiza
C. Siku ya sherehe
D. Siku ya kwaya

32. Siku ambayo walikuwa wanajitayarisha kwa siku hiyo, hutokea mara ngapi katika maoni yako mwenyewe?
A. Kila siku
B. Kila wiki
C. Kila mwezi
D. Kila mwaka

33. Ni vishamba vingapi vidogo vilitayarishwa?
A. Viwili
B. Kimoja
C. Vitatu
D. Hatujaelezwa

34. Hizi zote zilivunwa isipokuwa ______
A. maembe
B. mbegu za kabeji
C. mbegu za karoti
D. mbegu za nyanya

35. Wanafunzi ambao hawakutayarisha vijishamba ______
A. walikuwa wavivu.
B. walikuwa wameshatayarisha vyao.
C. waliadhibiwa
D. waliokota nyasi na kuteka maji

36. Ni kweli kusema ________
A. siku ya klabu haikufaulu
B. Bw. Odhis alikuwa mwalimu wa kupanda.
C. Bw. Odhis alikuwa mkulima
D. vijishamba vitano vilitengenezwa

37. Wanafunzi walitengeneza vijishamba ambavyo vilikuwa vimeinukia kwa ________
A. kumwagilia mchanga maji
B. kuinua mawe
C. kutumia nyasi zilizokauka
D. kuinua mchanga

38. Nani waliotayarisha vijishamba?
A. Bw. Odhis, Kageha na Ayaga
B. Ayaga peke yake
C. Ayaga, Kageha na mwandishi
D. Mwandishi na wana kikundi wengine.

39. Mbegu zilivunwa ______
A. katika vijishamba tofauti
B. kwa karatasi za nailoni.
C. kama zimechanganyika
D. kwa kutawanywa kila mahali

40. Nyasi zilizokusanywa zilikuwa za ____
A. kufanya vijishamba kuwa na joto
B. kuzuia vijishamba kuwa na joto
C. kuzuia panya
D. kunyunyizia vijishamba

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Bwana Pombe anaishi katika kijiji cha Mamboleo. Alipokuwa mtoto mdogo alipendwa sana na wazazi wake. Alikuwa na tabia nzuri sana. Lakini alipofika darasa la pili alianza kuwa mtoto mbaya sana. Alianza kuonjaonja sigara na kushiriki ulevi.

Bwana Pombe aliendelea na tabia hizo mbaya hadi akazoea na kuwa mlevi chakari wa kila siku. Alikatazwa lakini hakusikia. Alikataa kuendelea na masomo. Siku hizi Bwana

Pombe anateseka sana, hana makazi, hana pesa zozote za kugaramia mahitaji yake.

Anatamani kurudi shuleni lakini hawezi kukubaliwa kwani tabia zake ni potovu.

Yeye huishi sasa "ningalijua singalianza tabia mbovu. Kumbe elimu ni kitu kizuri! Maskini ningalijua!"

41. Bwana Pombe anaishi katika kijiji cha ________
   - A. Mbirikimo
   - B. Mbombolulu
   - C. Mamboleo
   - D. Kisasa

42. Ni lini alivyoanza tabia mbaya?
   - A. Akiwa mkubwa
   - B. Kabla kufikia darasa la tatu.
   - C. Akiwa darasa la tano
   - D. Hatujaambiwa

43. Ni ipi kati ya hizi tabia hakushiriki?
   - A. Uvutaji sigara
   - B. Ulevi wa kupindukia
   - C. Kutoenda shule
   - D. Wizi wa mabavu

44. Ni shida gani kubwa hasa ambayo imempata Bwana Pombe?
   - A. Kukosa mke
   - B. Kukosa bangi
   - C. Kukosa elimu
   - D. Kukosa ajira

45. Ni nini kinyume cha neno 'shida'?
   - A. Faida
   - B. Huzuni
   - C. Raha
   - D. Taabu

46. Hadithi hii inatufunza ______
   - A. ngoja ngoja huumiza matumbo
   - B. mtoto mtundu
   - C. elimu ndio ngao
   - D. ulevi hatari

47. Kuwa na tabia <u>potovu</u> ni ______
   - A. kufurahi sana
   - B. kuwa mvutaji sigara
   - C. kuwa na tabia mbaya
   - D. kuregarega

48. Neno 'chakari' limetumika katika habari hii linamaanisha ______
   - A. vizuri
   - B. kupindukia
   - C. hobelahobela
   - D. mmoja

49. Kwa nini Bwana huyu hawezi kurudi shuleni?
   - A. Ataadhibiwa na mwalimu
   - B. Ana umri mdogo
   - C. Hawezi kuelewa lolote
   - D. Tabia zake ni potovu.

50. Gani kati ya hizi si mbaya kwa afya?
   - A. Sigara
   - B. Tunda
   - C. Bangi
   - D. Pombe